## Kuelekea Tanzania ya Viwanda:

# Kuwekeza Katika Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki kwa Uhakika wa Huduma za Maji

EASTERN ARC MOUNTAINS CONSERVATION ENDOWMENT FUND
EAMCEF
MFUKO WA UHIFADHI WA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI

## Ujumbe Muhimu

- **25% ya idadi ya watu waishio katika mikoa ya nyanda za juu na nyanda za chini** ya Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania hutegemea maji ya mito ambayo vyanzo vyake ni Milima ya Tao la Mashariki.
- **90% ya umeme unaotokana na maji nchini Tanzania** huzalishwa katika vituo vikuu vya umeme vya Kidatu, Mtera, Kihansi, Nyumba ya Mungu, Pangani na Hale. Mabwawa katika vituo hivi hujazwa maji ambayo vyanzo vyake vipo katika Milima ya Tao la Mashariki.
- Uimarishaji wa uhifadhi wa misitu ya vyanzo vya maji katika nyanda za juu za Milima ya Tao la Mashariki una mchango mkubwa katika kupunguza gharama za uendeshaji wa vituo vya kuzalisha umeme zinazotokana na kufurika kwa mchanga katika mabwawa na katika miundominu ya usambazaji wa maji.
- Fedha za kutosha (na mikakati ya kifedha) zinahitajika ili kusaidia mamlaka za usimamizi wa misitu na jitihada za jamii zinazoshughulikia vyanzo vikuu vya uharibifu wa misitu ya vyanzo vya maji.
- Uwepo wa Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki na uzoefu wake katika kutafuta fedha na kutoa ruzuku ni fursa ya kuwezesha kupenyeza rasilimali kwa ajili ya ya uhifadhi wa milima ya Tao la Mashariki.

## 1. Utangulizi

**Andiko hili linasisitiza umuhimu wa kuimarisha uhifadhi wa misitu ya Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania kutokana na umuhimu wake mkubwa kama maeneo ya vyanzo vya maji.** Utajiri wa misitu iliyopo nchini Tanzania, hasa ile iliyo katika Milima ya Tao la Mashariki ni vyanzo muhimu vya maji. Kwa kuwa vyanzo vya maji, misitu hukusanya maji ya mvua na maji yanayotiririka na kuyaelekeza katika mito, mabwawa, maziwa au mfumo wa maji ya ardhini hivyo kudhibiti utiririkaji wa maji katika mfumoikolojia kwa wakati wote. Maji kama huduma muhimu ya mazingira ni muhimu kwa ajili ya uendelevu wa biaoanuwai zilizopo na kwa shughuli za binadamu - iwe ni kwa shughuli za nyumbani, kilimo au viwandani.

**Serikali ya Tanzania imeweka mifumo mizuri ya kisera ili kuwezesha usimamizi na uhifadhi wa maji.** Kwa mfano, Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inatambua umuhimu wa misitu katika kuhifadhi vyanzo vya maji na inasisitiza umuhimu wa kutunza maji kama rasilimali iliyomo hatarini inayokabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa mahitaji kutoka katika sekta mbalimbali yanayotokana na ongezeko la kasi la idadi ya watu, uharibifu wa mazingira, kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kama vile ongezeko kubwa la kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji viwandani, uzalishaji wa umeme wa maji, uchimbaji wa madini, ufugaji, uvuvi, usafi wa mazingira na maji kwa ajili ya matumizi ya wanyamapori. Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 ina lengo kuu la kuhakikisha kwamba mchango wa sekta ya misitu katika maendeleo ya taifa unaimarishwa wakati huohuo ikihifadhi na kuendeleza usimamizi wa maliasili.

**Mpango wa III wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 -2025/2026) wa Juni 2021 unahamasisha uhifadhi na matumizi endelevu ya ardhi kwa ajili ya usimamizi wa maji ikijumuisha matumizi ya mbinu jumuishi.** Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 2021 na andiko la Nationally Determined Contributions (NDC) la mwaka 2021 linaelezea uhifadhi wa maji katika muktadha wa mabadiliko ya tabianchi na kuainisha mikakati muhimu ya kujenga uhimilivu katika sekta ya maji, ikijumuisha kupitia usimamizi endelevu wa misitu ya vyanzo vya maji.

**Pamoja na uwepo wa nyenzo za kisera na kutoa kipaumbele katika usimamizi wa maji katika ngazi ya taifa, fedha za kutosha zinahitajika ili kuwezesha uhifadhi wa vyanzo vya maji na kuwa na uendelevu na uhimilivu wa huduma za maji**.

## 2. Misitu ya Milima ya Tao la Masharíki na Huduma za Maji

Milima ya Tao la Mashariki ni chanzo muhimu cha maji kwa mito inayotoka katika milima hiyo ikitegemewa na takribani 25% ya idadi ya watu nchini Tanzania. Mito mingi ya Mashariki mwa Tanzania hujipatia maji yake kutoka katika vyanzo vya Milima hiii. Maji yanayoanzia katika milima hii hutumika kwa kiasi kikubwa katika katika kuzalisha umeme, shughuli za kilimo cha mazao ya chakula na mazao ya biashara (kwa mfano, mpunga, mahindi, miwa, mazao ya misitu, chai, kahawa n.k.), matumizi ya nyumbani na viwandani – kama ilivyoelezezwa katika mifano michache hapa chini:

**Maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na viwandani:** Milima ya Uluguru ni chanzo cha maji ya Mto Ruvu ambao husambaza kiasi kikubwa cha maji yake katika mikoa mitatu ya Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam. Mto Ruvu umeingia katika Mto Ngerenge, ambao chanzo chake cha maji ni ukanda wa kaskazini mwa Milima ya Uluguru na hupeleka maji yake katika mji wa Morogoro. Milima ya Usambara Mashariki (katika Misitu ya Hifadhi Asilia ya Amani na Milima ya Handei) ni vyanzo vya Mto Zigi unaosambaza maji yake katika mkoa wa Tanga. Mito ya Wami, Kilombero, Mto Ruaha Mdogo, na Pangani pia hutiririsha maji yake kuelekea sehemu mbalimbali na kuwa chanzo kikuu cha maji kwa shughuli za vijijini, shughuli za kilimo cha mashamba makubwa na viwanda katika nyanda za chini za Milima ya Tao la Mashariki. Miji na majiji ya Dodoma, Iringa, Tanga, Dar-es-Salaam, Morogoro, Ifakara, Lushoto, Mwanga, Same, Mombo, Korogwe, Soni, Kilosa, Muheza, Kibaha, Mpwapwa, Mvomero, Turiani, Kilindi, Gairo, Mikumi, Chalinze, Handeni na Kilolo hutegemea maji ambayo vyanzo vyake vipo

katika Milima ya Tao la Mashariki.

**Maji kwa ajili ya umeme:** Milima ya Tao la Mashariki ni chanzo kikuu cha zaidi ya 90% ya umeme unaotokana na maji unaozalishwa katika vituo vikuu vya umeme. Kwa mfano, mito inayoanzia katika Bloku za Milima ya Udzungwa hutiririsha maji yake kuelekea katika vituo vya kuzalisha umeme vya Kidatu na Mtera vilivyopo katika Mto Ruaha Mkuu. Mito hii hulisha pia kituo cha kuzalisha umeme cha Kihansi (kilichopo katika Mto Kihansi). Bloku za Milima ya Pare Kaskazini, Pare Kusini na pare Magharibi hupeleka maji yake katika maporomoko ya Pangani, vituo vya kuzalisha umeme vya Hale na Bwawa la Nyumba ya Mungu. Kwa muda mrefu, Bwawa la kuzalisha Umeme la Mwalimu Julius Nyerere lililoko katika bonde la Stiegler limekuwa likiangaliwa kama sehemu muhimu kwa uzalishaji wa umeme. Eneo hili hutegemea maji ambayo vyanzo vyake ni Milima ya Tao la Mashariki. Jumla ya thamani ya kiuchumi ya umeme unaotokana na maji kutoka katika mfumoikolojia wa Milima ya Tao la Mashariki inakadiriwa kuwa Dola za Marekani bilioni 66 ambayo ni sawa na 28% ya jumla ya thamani ya kiuchumi ya mfumoikolojia wote.

**Maji kwa ajili ya shughuli za kilimo:** Mfumoikolojia wa Milima ya Tao la Mashariki una mazingira yanayofaa sana kwa shughuli za kilimo; yaani udongo, virutubisho, maji na hali ya hewa inafaa kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara yanayotumika nchini na nje ya nchi. Kilimo cha mashamba makubwa ya mazao ya biashara yaliyoko katika mfumoikolojia wa Milima ya Tao la Mashariki kina mchango mkubwa katika uchumi wa taifa kwa mazao kama vile kahawa, mkonge, chai na miwa. Mashamba makubwa ya miwa ya Kilombero na Mtibwa yanafaidika kwa ardhi na hali ya hewa ya Milima ya Tao la Mashariki. Jumla ya thamani ya kilimo kiuchumi (ikijumuisha ufugaji) inakadiriwa kuwa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 4. Ndani ya mfumoikolojia wa Milima ya Tao la Mashariki serikali imedhamiria kutenga takribani Kilometa za Mraba 287,00 kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji wa ubia na binafsi katika sekta ya kilimo kupitia kilimo cha umwagiliaji. Eneo hili hujulikana kama eneo la Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini (SAGCOT). Eneo la SAGCOT linaingiliana katika bloku nane za Milima ya Tao la Mashariki ambazo ni nyanda za juu za milima ya Nguu, Nguru, Uluguru, Ukaguru, Rebeho, Malundwe, Udzungwa na Mahenge. Pamoja na mambo mengine milima hii ni chanzo cha maji kwa mabonde ya mito katika sehemu kubwa ya ardhi inayodhamiriwa katika Mpango wa SAGCOT. kwa mfano, Bonde la Mto Ruaha/Rufiji lenye mabonde madogo ya Mto Ruaha Mkuu, Kilombero na Luwego na ardhi oevu ya bonde la Kilombero, Usangu, Delta ya Rufiji hutiririsha maji yake katika sehemu kubwa ya ukanda wa SAGCOT. Mito mingine iliyopo katika ukanda huo ni pamoja na Bonde la Wami/Ruvu, Bonde la Ziwa Rukwa na Ziwa Nyasa.

## 3. Ajenda ya Viwanda na Maji –Kuna Uhusiano Gani?

Tangu serikali ya Tanzania ilipojiwekea Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, imekuwa ikitekeleza miradi mbali mbali ya kimkakati ili kufikia malengo ya kuwa nchi ya uchumi wa kati. Hata hivyo, tangu Julai 2020 nchi imepata hadhi ya uchumi wa kati wa chini. Hivyo, ajenda ya viwanda imepewa kipaumbele ili kuongeza ukuaji na mabadiliko na kwa kiasi kikubwa inatekelezwa kupitia mipango ya maendeleo ya miaka mitano. Mipango yote ya Maendeleo yaani Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/1017-2020/2021) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022-2012/2026) imeweka jitihada za kimkakati kwa sekta mbalimbali ili kuchochea manufaa ya kijamii na kiuchumi katika ngazi ya taifa. Ajenda ya viwanda inaweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuongeza uwekezaji katika sekta muhimu ikijumuisha kuongezeka kwa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Kuongezeka kwa shughuli za viwanda inamaanisha kuongezeka kwa matumzi ya malighafi, matumizi ya umeme na rasilimali nyingine muhimu. Rasilimali za viwanda kama vile maji yanayotokana na vyanzo vya ardhini kama mito, maziwa, mabwawa na chemchem kwa kawaida hayatiliwi maanani sana kutokana na upatikanaji wake wa kiasili na kuwa na thamani ndogo.

Kwa kuelewa umuhimu wa kiuchumi wa Milima ya Tao la Mashariki kama vyanzo vya maji kwa mikoa ya jirani na jamii zinazoishi nyanda za chini, ni dhahiri kwamba kuongezeka kwa shughuli za viwanda kunaongeza mahitaji ya maji. Njia mojawapo ya kuhakikisha upatikanaji endelevu wa huduma za maji kutoka katika mfumoikolojia ni kuimarisha uhifadhi wa misitu ya vyanzo vya maji ya Milima ya Tao la Mashariki. Hatua za kuimarisha uhifadhi zinamanisha kuongeza fedha na uwezo wa taasisi zinazosimamia misitu, kuongeza uwekezaji katika mbinu za kusimamia ardhi ambazo zitasaidia jamii zinazoishi nyanda za juu, ikijumuisha kupitia shughuli mbadala za uzalishaji kipato wakati huohuo kushughulikia vyanzo vikuu vya ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu. Njia mojawapo ya kushughulikia tatizo la ukosefu wa fedha katika usimamizi wa misitu ni kuandaa na kutekeleza mkakati madhubuti wa ufadhili katika misitu (forest financing strategy) ambao utasaidia taasisi na wizara zinazohusika kunufaika na fursa za fedha za kitaifa na kimataifa.

## Kuhusu Mfuko wa Uhifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF)

Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) ni Mfuko wa udhamini ulioanzishwa na unaofanya kazi kama mkakati wa muda mrefu na wa uhakika wa ufadhili wa shughuli za maendeleo ya jamii, tafiti za uhifadhi na kuendeleza bioanuwai, huduma za kiikolojia na matumizi endelevu ya maliasili katika Milima ya Tao la Mashariki iliyoko nchini Tanzania. EAMCEF hufanya kazi kama Asasi isiyo ya Serikali isiyo ya Biashara, hutafuta fedha na hutoa ruzuku kwa Idara za Serikali (Serikali kuu na Serikali za Mitaa), Asasi Zisizo za Serikali, Wanajamii, Taasisi za Utafiti, Taasisi za Elimu, Kampuni Binafsi pamoja na watu binafsi.

**Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:**

**Sekretarieti ya EAMCEF,**
Kiwanja Na. 348, Eneo la Forest Hill, Barabara ya Kingalu,
S.L.P. 6053, Morogoro, Tanzania.
Simu ya Mezani: +255 (0) 23 2934274.
Simu ya Mkononi: +255 (0) 755 330558.

**Barua Pepe:** eamcef@easternarc.or.tz.
**Tovuti:** www.easternarc.or.tz
**Twitter:** www.twitter.com/eamceftanzania
**Instagram:** www.instagram.com/eamceftanzania
**Facebook:** www.facebook.com/eamcef